
Jarida la
# MBULU YETU
Maendeleo kwanza

LIMEANDALIWA NA OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI HALMASHAURI YA MBULU | TOLEO #. 01 | MACHI 2020





## MIAKA MITANO YA UPEPO WA "KISULISULI" CHA MAENDELEO KATIKA HALMASHAURI YA MBULU














## Uchaguzi serikali za mitaa 2019 CCM yapasua "anga" Mbulu

# YALIYOMO


| | | |
|---|---|---|
| 01-02 | - | Ziara ya Kamati ya Bunge |
| 03 | - | Ujenzi |
| 04 | - | Mazingira |
| 05 | - | Afya |
| 06 | - | Utumishi |
| 07 | - | Sheria |
| 08-09 | - | Kilimo na Ushirika |
| 10 | - | Elimu-msingi |
| 11 | - | Elimu-Sekondari |
| 12 | - | Ustawi wa Jamii (TASAF) |
| 13 | - | Ustawi wa Jamii (AFYA) |
| 14 | - | Utumishi na Utawala |
| 15 | - | Fedha na Mipango |
| 16 | - | Kitengo ch Uchaguzi |
| 17 | - | Ardhi & Maliasili |
| 18 | - | Ardhi & Maliasili |

# ZIARA YA KAMATI YA BUNGE YA SERIKALI ZA MITAA HALMASHAURI MBULU.........

## HABARI PICHA



01

Mwenyekiti wa Kamati Ya Bunge ya Serikali za Mitaa (MB) Dkt. Jasson Rweikiza akiwa ameongozana na wajumbe wa kamati hiyo wakielekea kukagua jengo la huduma ya mama na motto katika ujenzi wa hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu



02

Naibu Waiziri wa OR- TAMISEMI (MB) Mhe Mwita Waitara, wakwaza kulia akiteta jambo na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mbulu Hudson Kamoga, mwenye koti jeusi



03

Kutoka kulia ni Naibu Waiziri wa OR-TAMISEMI (MB) Mhe. Mwita Waitara, Mbunge wa jimbo la Manyoni Mashariki Mhe. Daniel Mtuka, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mbulu Hudson Kamoga, Mbunge wa jimbo la Kilolo Mhe. Venance Mwamoto na Mbunge wa jimbo la Kelwa Mhe. Innocent Bilakwate.



04

Mwenyekiti Wa Kamati Ya Bunge Ya Serikali Za Mitaa Dkt. Jasson akiwa akinaw mikono baada ya kupanda mti wa matunda ikiwa ni ishara ya ukumbusho baada ya kumaliza ziara ya ukaguzi wa Ujenzi wa hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, kutoka kulia ni Mganga wa mkuu wa hospitali hiyo Dkt Boniventure

05

Mwenyekiti Wa Kamati Ya Bunge Ya Serikali Za Mitaa Dkt. Jasson Rweikiza akiwa katika picha ya pamoja Naibu Waziri wa OR-TAMISENI Mhe. Mwita Waitara, na wajumbe wa kamati hiyo mara baada ya ziara ya ukaguzi wa ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu ambayo ni moja kati ya hospitali za Wilaya 67 za awamu ya kwanza iliyojengwa nchini kwa sh. Bil 1.5 kila moja.



## HABARI KATIKA PICHA



06

Mjumbe wa Kamati Ya Bunge Ya Serikali za mitaa na Mbunge wa jimbo la Mpwapwa Mhe. George Lubeleje.



07

Mwenyekiti Wa Kamati Ya Bunge Ya Serikali Za Mitaa Dkt. Jasson (wa kwanza kulia) akisikiliza maelezo ya Naibu Waziri wa OR-TAMISEMI Mhe. Mwita Waitara (wa pili kulia), Katibu Tawala wa mkoa wa Manyara Ndg. Masaile Mussa pamoja na watumishi wengine wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu



08

Mbunge wa Manyoni Mashariki Mhe. Daniel Mtuka (aliyeshika simu), Mbunge wa jimbo la Kilolo Mhe. Innocent Bilakwate (wa pili kulia) pamoja na Afisa Tehama Ndg. Nyanda Komanya wakiwa katika picha ya pamoja

Mwenyekiti ka kamati ya Bunge ya Serikali za Mitaa Dkt. Jasson (wa pili kulia) akiwa pamoja na Naibu Waziri wa OR-TAMISENI Mhe. Mwita Waitara (wa kwanza kushoto), pamoja na Katibu Tawala mkoa wa Manyara Ndg. Masaile Mussa.

09





10

Naibu Waziri wa OR-TAMISENI Mhe. Mwita Waitara (wa pili kulia), Katibu Hospitali ya Wilaya ya Mbulu Dkt. Isondo (wa kwanza kulia) pamoja na wana kamati wengine wa CHMT Wilaya ya Mbulu, Monica Shauri (wa kwanza kushoto) anayefuata ni Pellagia Shirima

# Ujenzi unavyofanya kazi ya kuimarisha miundombinu ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu

HABARI KATIKA PICHA



01 Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu Mhe. Joseph Mandoo aliyeketi kwenye kiti kushoto. Mkurugenzi mtendaji Hudson Kamoga pamoja na watumishi wengine wakipokea maelezo ya mchoro wa jengo la Halmashauri



02 Muonekano wa juu wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu ambao ni moja kati ya hospitali za Wilaya 67 za awamu ya kwanza iliyojengwa nchini kwa sh. Bil 1.5 kila moja. Jengo la mbele ni jingo la mama na mtoto (maternity ward).



03 Mhandisi wa Halmashauri ya Wilaya Mbulu Samweli Bundala (aliyerudisha mikono nyuma) pamoja na wahandisi kutoka kampuni ya ujenzi ya DIT kwa pamoja wakihakiki miundombinu na vifaa vilivyotumika katika ujenzi.



04 Mhandisi wa Halmashauri Samweli Bundala akihakiki vipimo katika jingo la halmashauri



05 Muonekano wa nyuma wa jengo la utawala la Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu kwa sasa liko hatua ya asilimia 87 kukamilika, ambapo Jengo hilo la Utawala limekadiriwa kujengwa kwa gharama ya Tsh 6.7 ambapo gharama za ujenzi ni Bil 6.3 na gharama sa mhandisi mshauri ni mil 351 huku gharama sa kuandaa mchoro zikigharimu tsh mil 30



06 Muonekano wa jengo la maabara katika kituo cha afya Dongobesh

Ujenzi wa ukarabati wa Kituo cha afya cha Dongobesh ambapo Serikali ilituma kiasi cha sh. mil. 400, ambapo tayari kimeanza kufanya kazi toka oktoba 2019, huku jengo la wagonjwa wa nje (OPD) ambapo inatarajiwa kufanya kazi mapema mwaka huu 2020.

Ujenzi wa hospitali ya halmashauri ya Wilaya ya Mbulu ambapo serikali ilipeleka jumla ya sh. Bil. 1.5, pia ujenzi wa jengo jipya la utawala la halmashauri ya Wilaya hiyo lilofikia asilimia 70 hadi hivi sasa ambapo zaidi ya sh. bil.2.5 zimetumika.

Katika jengo hilo la utawala kwani kwa sasa liko hatua ya asilimia 87, jengo la matenite ambalo liko asilimia 85, jengo la stoo ya madawa liko asilimia 99, jengo la maabara liko asilimia 90, jengo la kufulia liko asilimia 95 na huku jengo la mionzi likiwa liko asilimia 98 na kinahitajika kiasi cha sh. mil. 338,153,270

# WAHADZABE wanufaika na utunzaji wa mazingira, jumla ya miche Mil. 2,800,000 imepandwa

## HABARI KATIKA PICHA

Afisa Usafi na Mazingira wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, Juma kingu Kilimba akielezea mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka mitano (2015- 2020) cha awamu ya tano ya Rais Dkt. John Pombe Magufuli, Kilimba anasema ni kuunganisha jamii zinazohifadhi misitu ya jamii na wadau ambapo katika vijiji vya Mongo wa Mono, Yaedachini na Domanga vimeingia katika mikataba na hewa ya ukaa (Carbon Tanzania – CT LTD), ambapo malipo ya hewa ya ukaa kila kijiji hujipatia zaidi ya sh. Mil. 27 kila baaada ya miezi sita, hivyo kila kijiji hujipatia sh. Mil. 54 kwa mwaka mmoja, kwa miaka mitano ya mh. Dkt. Magufuli vijiji hivyo vitatu vimepata jumla ya



01 Moja ya misitu mikubwa iliyopo katika eneo la Wahadzabe Yaedachini



02 Mkurugenzi mtendaji Hudson Kamoga pamoja na watumishi wa halmashauri ya Wilaya ya Mbulu katika picha ya pamoja baada ya kupanda miti



03 Aliyekuwa Katibu Mkuu Wizara ya Habari Utamaduni Sanaa na Michezo Bi. Suzan katikati na Kaimu Mkurugenzi wa Utamaduni Wizara ya Habari Sanaa na Utamaduni Bi. Liliano Beleko wa pili kutoka kushoto wakicheza ngoma na akina mama wa jamiii ya Wahadzabe katika kijiji cha Dumanga.

Halmashauri ya Wilaya imeweka utaratibu wa kupanda miti na kusimamia kikamilifu katika maeneo mbali mbali ya wazi, maeneo ya umma, nay a watu binafsi, ambapo kwa kipindi cha miaka mitano (2015 – 2020) jumla ya miti ipatayo mil. 2,800,000 imepandwa.

Athuman Magandula ni mkazi wa Kijiji cha Domana kata ya Yaeda Chini, anaeleza mafanikio waliyoyapata kutokana na kuhifadhi misitu, kuwa vijiji vitatu vya Yaedachini, Domanga na Mongowamono vinenufaika na hewa ya ukaa kutoka kwa wadau wa mazingira ambapo kila mwaka kila kijiji hupata sh. Mil. 54.



04 Aliyekuwa Katibu Mkuu Wizara ya Habari Utamaduni Sanaa na Michezo Bi. Suzan Mlawi akitoka katika moja ya nyumba ya familia ya kihdzabe.



05 Mkurugenzi mtendaji Hudson Kamoga pamoja na Mganga mkuu wa hospitali ya halmashauri ya Wilaya Dkt. Boniventure Chitopela wakipanda mti katika hospitali ya wilaya

# HUDUMA ZA AFYA Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu zinavyonufaisha jamii

HABARI KATIKA PICHA



01

Wataalam wa maabara ya kituo cha afya Dongobesh wakikagua mashine ya kumpatia motto joto mara baada ya kuzaliwa ((infrant radiant warmer)

Dkt Bonaventure Chitopela anasema idara ya afya ina vituo vya kutolea huduma za afya zipatazo 30 ambapo kuna hospitali mbili moja ya rufaa ya Haydom inayomilikiwa na (KKKT) Dayosisi ya Mbulu huku serikali ikiwa na ubia kwenye hospitali hiyo na hospitali ya mpya ya Wilaya ya Mbulu iliyopo makao makuu ya halmashauri hiyo kata ya Dongobesh ambayo imeanza kutoa huduma kwa wagonjwa wa nje, huku vituo vya afya kwenye halmashauri ya wilaya hiyo ni viwili na zahanati 26.




04

Baadhi ya wafanyakazi wa kigeni katika hospitali ya Hydom kutoka mataifa rafiki



05

Katibu wa Hospitali ya halmashauri ya wilaya ya Mbulu Dkt. Isondo (wa kwanza kulia). Muuguzi wa zamu katika kituo cha afya Dongobesh (aliyeshika karatasi) wakimjulia hali mgonjwa wa kwanza kufanyiwa upasuaji kituo .

Kuhusu dawa na vifaa tiba wameongeza dawa na vifaa tiba vya kisasa toka asilimia 70 mwaka 2015 hadi asilimia 95 kwa mwaka 2020. Na kuhusu miundombinu serikali imeimarisha miundombinu ambapo katika halmashauri hiyo serikali imetoa kiasi cha shilingi bilioni 1.9 ambapo shilingi milioni 400 ni kwa ajili ya kukarabati kituo cha afya Dongobesh, na shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali mpya ya wilaya inayomilikiwa na halmashauri ya wilaya ya Mbulu.




05

Zahanati ya Medawi iliyokuwa imeezuliwa na kimbunga ikiwa tayari imekamilika baada ya marekebisho na sasa huduma ya afya iaendelea kutolewa kama kawaida



07

Jengo la wodi ya mama na mtoto katika kituo cha afya Dongobeshi,

"Kwa sasa huduma kwenye idara ya afya zimeboreshwa halmashauri ya wilaya ya Mbulu kwani kwa upande wa wakiwa mama wajawazito miaka iliyopita tulikatazwa kuzalia mimba ya kwanza kwenye kituo cha afya Dongobesh ila hivi sasa baada ya kuboreshwa wanawake wajawazito wanazalishwa tuu hata kama ni ujauzito wa kwanza," mkazi wa kata ya Dongobesh Stella Mshanga (45)



05

Mashine ya kuulia vijidudu/bakteria (Sterilizer machine) kabla na baada ya upasuaji katika nguo ili kuepusha maambukizi mapya

# Wazee 8000 wapatiwa vitambulisho vya matibabu bure Mbulu.

HABARI NA PICHA

Mafanikio yaliyopatikana ndani ya miaka mitano ya awamu ya tano ya Dkt. Magufuli kuwa ni pamoja na kuwapatia wazee 8000 vitambulisho vya msamaha matibabu kwa kata zote 18 na vijiji 76 kwa Wazee wote wenye umri wa miaka 60 na kuendelea, ambao wanahudumiwa na vituo vyote vya serikali.

Afisa Ustawi wa Jamii Ezekiel Assecheck anasema wamefanikiwa kuunda baraza la wazee litakaloshughulikia kutatua matatizo ya wazee kwa ngazi zote za kijiji, kata na ngazi ya wilaya na zinafanya kazi vizuri, Baraza ambalo miaka mitano ya nyumba haikuwepo, ambapo katika kitengo hiki kesi zote za watoto hufikishwa mahakama ya watoto kwa wakati na Afisa Ustawi wa Jamii huusishwa kuanzia kesi inaposikilizwa hadi kupatiwa hukumu na kuhusishwa kwenye vikao vyote vya mahakama kuhusiana nankesi husika.

Mmoja wa wazee Paulo Jiorojick (65) anaipongeza serikali ya awamu ya tano ya mh Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuwakumbuka wazee, kwani wanapata huduma mbalimbali za afya bure, mapango huu ni mzuri sana ambao awali haukuwepo na kila mtu aliyezaliwa atakua ni mzee mtarajiwa kwa uwezo wa Mungu"




01

Mmoja wa wazee walionufaika na kadi za bima ya afya kupata matibabu bure mzee Atanasio Gethami katika zoezi la kupiga picha



02

Katika kijiji cha Bashay wakikusanya data kutoka kwa wazee wa eneo hilo ili kuingiza katika mfumo wa kupata kadi za afya




03

Afisa kutoka idara ya afya akimsaidia mama kuweka sahihi ya kidole katika fomu

# KITENGO CHA SHERIA KUKABILIANA NA UPOTEVU NA UHARIBIFU WA NAFAKA

**HABARI KATIKA PICHA**

Gwandumi Mwamba anaeleza jinsi kitengo cha sheria kilivyofanikiwa katika kipindi cha awamu ya tano ya serikali chini ya Rais Dkt. John Pombe Magufuli kuwa kitengo kilifanikiwa kuiwakilisha halmashauri kwenye vyombo mbalimbali vya kisheria amabapo mashauri mbalimbali hasa ya ardhi yalikwisha bila kuleta madhara (bila kuiingizia halmashauri hasara)

"Mafanikio mengine yaliyopatikana ndani ya miaka hii mitano 2015-2020 kitengo kilifanikiwa kuanzisha mchakato wa kutunga sheria ndogo ya mwaka 2019 na sheria ndogo ya ada na ushuru ya (Tangazo la serikali Na. 842 la Novemba 8, 2019) juu ya kuzuia utotevu na uharibifu wa nafaka wakati na baada ya kuvuna"

Hata hivyo Mwamba anasema mbali hayo pia Kitengo hiko kimefanikiwa kuiwezesha Halmashauri kuingia mikataba mbalimbali ikiwemo ya ujenzi wa miundombinu mbalimbali ikiwemo ya barabara,



01

Mwanasheria wa halmashauri ya Wilaya ya Mbulu Ndg. Gwandumi Mwamba



02

Kikao cha baraza la madiwani kikiongozwa na mwenyekiti wa halmashauri ya wilaya mbulu Mhe. Joseph Mandoo wa pili kutoka kushoto

"Tunasimamia na tunashauri utendaji kazi wa mabaraza ya kata na kutoa elimu ya katiba na haki za kiraia kwa raia wote katika ngazi ya halmashauri" anasema Gwandumi.

"Mafanikio yaliyopatikana ndani ya miaka hii mitano kitengo kilifanikiwa kuanzisha mchakato wa kutunga sheria ndogo ya mwaka 2019 na sheria ndogo ya ada na ushuru juu ya kuzuia upotevu na uharibifu wa nafaka wakati na baada ya kuvuna"

# Kilimo kinavyowanufaisha wananchi wa Halmashauri ya Mbulu

## HABARI KATIKA PICHA



01 Mmoja wa wakulima wa zao la vitunguu ndugu Hando Bura akianika vitunguu maji tayari kwa kuingiza sokoni



02 Wakazi wa kijiji cha Dongobesh wakimenya maharage

Kilimo na Umwagiliaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu Yustina Arcadius Rahhi anasema mazao ya Chakula yanayolimwa ni pamoja na Mahindi, Maharage, Mtama, Viazi vitamu, Viazi Mviringo, Ndizi, Kunde, Mihogo, Ngano na Ulezi. Mazao ya biashara yanayolimwa ni pamoja na Alizeti, Vitunguu Saumu, Vitunguu Maji, Ngwara na Mbaazi.

Jumla ya wakulima 33,712 waliweza kupata mafunzo mbalimbali ya teknolojia na mbinu rahisi zenye kufanya kilimo chenye tija kwa nadharia na vitendo. Mafunzo haya yametolea kupitia warsha, semina, mikutano ya hadhara, maonesho ya nane nane, kituo cha Radio Habari Njema, mashamba darasa na mashamba ya mfano.

Kwa wastani uzalishaji wa mazao ya chakula umeongezeka kutoka tani 59,216 mwaka 2016 hadi 71,969 mwaka 2019" anasema Rahhi.

"lakini pia kuongezeka kwa mnyororo wa thamani ambapo wakulima wamekuwa wakichakata na kusindika zao la vitinguu saumu kwenye kiwanda kidogo cha Bashay na kuuza kwenye maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi ambapo uzalishaji umeongezeka kutoka tani 2 hadi tani 3.8 kwa mahindi, tani 0.8 hadi 2 kwa hekta maharage, na tani 3.0 hadi tani 9 kwa hekta



04 Wataalam wakikagua maendeleo ya mradi wa bwawa la umwagiliaji Dongobesh ambalo hutumika kwaajili ya matumizi ya kilimo cha mazao chenye tija kisichotegemea mvua za msimu



03 Mkurugenzi mtendaji Hudson Kamoga akikagua maendeleo ya ujenzi wa mfereji wa bwawa la umwagiliaji katika kata ya Dongobesh



Muonekano wa shamba la papai lililopo katika halmashauri yetu katika kata ya Hydom 06



05 Mafundi wakiendelea na ujenzi wa mfereji wa kupitisha maji kwaajili ya kilimo

## HABARI NA PICHA

Mradi wa ujenzi wa bwawa la Dongobesh umekamilika mwaka 2020 ambapo umegharimu kiasi cha sh 2,354,360,563. Aidha ameongezea kuwa katika kipindi cha awali kabla ya kupata mradi uzalishaji kwa wakulima ulikuwa mdogo kwani maji mengi yalikuwa yanapotea njiani (seepage & evaporation) kabla ya kufika shambani na hivyo wakulima walikuwa hawapati maji ya kutosha kwa ajili ya kumwagilia mazao yao.

Kufuatia bwawa hilo wakulima wameweza kuboresha maisha yao kwa kuongezeka kipato ambacho kimewafanya wajenge nyumba nzuri za bati, waweze kuwasomesha watoto wao, kupata huduma bora za afya na pia kupata uhakika wa chakula bora ndani ya familia.



07

Mkurugenzi mtendaji Hudson Kamoga akiwa na wataalam wa kilimo kutoka Taasisi ya utafiti wa kilimo Arusha wakiangalia na kutoa elimu kwa wakulima Wilayani Mbulu kuhimiza matumizi ya mbegu bora ili kuongeza uzalishaji katika zao la maharage



08

Muonekano wa shamba la kilimo cha maharage ambalo limenufaika na ujenzi wa bwawa



09

Wakulima wa zao la vitunguu maji wakiwa shambani wakiendelea kukagua maendeleo ya zao hilo

"lakini pia kuongezeka kwa mnyororo wa thamani ambapo wakulima wamekuwa wakichakata na kusindika zao la vitinguu saumu kwenye kiwanda kidogo cha Bashay na kuuza kwenye maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi ambapo uzalishaji umeongezeka kutoka tani 2 hadi tani 3.8 kwa mahindi, tani 0.8 hadi 2 kwa hekta maharage, na tani 3.0 hadi tani 9 kwa hekta vitunguu saumu".



11

Kilimo cha alizeti ni moja zao kubwa linalolimwa ukanda huu katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, hapa ni katika shamba lililoko Dongobesh

# MIRADI IDARA YA ELIMU MSINGI

HABARI NA PICHA

Mafanikio hayo yanatokana na sera ya Elimu bila malipo ambapo seriakali imekua ikituma fedha kila mwezi katika akaunti ya kila shule ili kugharamia ambapo kwa mwaka 2016/2016 kwa mwaka mzima ziliingia jumla ya sh. Mil. 165,632,742.34, mwaka 2016/2017 sh mil. 986,822, 418.00, mwaka 2017/2018 sh. Mil. 714,812,204.00, mwaka 2018/2019 sh. Mil. 837,946,783.00 huku mwaka 2019 hada February 2020 wametuma sh. Mil. 645,364,924.00.



01

Ujenzi wa Darasa Moja na Ofisi Ya Walimu katika shule ya msingi Hydom

Mwaka 2015 kulikuwepo na shule 94 huku 2020 ziko shule 96 ongezeko ni shule mbili sawa na asilimia 2.1 , Uandikishaji wa wanafunzi mwaka 2015 walikua wanafunzi 4,660 wakati mwaka 2020 ni wanafunzi 6,833 ongezeko ni wanafunzi 2,173 sawa na asilimia 31.8.

Kwa upande wa hali ya ufaulu katika matokeo ya darasa la saba (PSLE) mwaka 2015 walifaulu kwa asilimia 56 wakati 2020 walifaulu kwa asilimia 72.6 ongezeko likiwa ni asilimia 16.6 sawa na asilimia 16.6, ufaulu wa darasa la nne [SFNA] kwa mwaka 2015 hali ya ufaulu ulikua ni wa asilimia 88.5 , wakati mwaka 2020 walifaulu kwa asilimia 95 ongezeko likiwa ni asilimia 6.5 sawa na asilimia 6.5, huku vitabu vya kiada (uwiano) kwa mwaka 2015 kitabu kimoja kilikua kinasomwa na wanafunzi 6 (1:6) wakati mwaka mwaka 2020 kitabu kimoja kinasomwa



02

Ujenzi wa darasa moja katika shule ya msingi Arri iliyopo kata ya Tumati



03

Ujenzi wa madarasa mawili, matundu sita ya choo katika shule ya msingi Muslur iliyopo Dinamu



04

Ujenzi wa madarasa moja katika shule ya msingi Endagulda

# MIRADI IDARA YA ELIMU SEKONDARI

HABARI NA PICHA

Mafanikio ya idara yake katika kipindi cha miaka mitano kutoka 2016 hadi 2020, idadi ya shule za sekondarikwa mwaka 2015 zilikua 19 na kufikia 22 na kuongezeka 3 sawa na asilimia 14, maabara ya masomo ya sayansi zilikua 9 kwa mwaka 2015 hadi kufikia 17 mwaka 2020 hivyo ongezeko ni 8 sawa asilimia 47.

Ongezeka kwa mabweni ya wasichana kutoka 15 kwa mwaka 2015 hadi kufikia 16 mwaka 2020 ongezeka ni bweni 1 sawa na asilimia 6, madarasa yalikua 185 hadi kufikia 211 kwa mwaka 2020 ongezeko yakiwa ni madarasa 26 sawa na asilimia 12, kwa mwaka 2015 nyumba za walimu zilikua 77 wakati 2020zikiwa nyumba 97 na kufanya ongezeko la nyumba 20 sawa na asilimia 21 , huku ongezeko yakiwa ni madarasa 3 sawa na asilimia 14, matundu ya vyoo 2015 yalikua ni 213 ukilinganisha na matundu ya vyoo 316 kwa mwaka 2020 ongezeko likiwa ni 103 sawa na asilimia 33.



01

Ujenzi wa darasa moja na stoo na katika shule ya sekondari Yaedachini iliyopo kata ya Yaedachini



02

Ujenzi wa darasa moja na stoo na katika shule ya sekondari Yaedachini iliyopo Yaedachini

mwaka 2015 ufaulu wa kidato cha nne umeonezeka kutoka asilimia 69 .7 hadi kufikia asilimia 85.4 ya mwaka 2019, huku ufaulu wa matokeo ya kidato cha sita ya mwaka 2015 yakiwa ni asilimia 100 wakati mwaka 2019 ni asilimia 99.2. mtihani wa kidato cha pili mwaka 2016 wanafunzi walifaulu kwa asilimia 95.7 wakati mwaka 2019 walifaulu kwa asilimia 95.6, ambapo hali ya uandikishaji wa kidato cha mwaka 2015 ni wanafunzi 1,588 ukilinganisha na 2020 wanafunzi 2,490





03

Ujenzi wa madarasa mawili katika shule ya sekondari Tumati iliyopo kata ya Tumati

# TASAF: “watoto 8 kutoka kaya maskini wamejiunga vyuo vikuu”

HABARI NA PICHA

Mratibu wa Mradi wa Tasaf wilaya ya Mbulu, mkoani Manyara Mosses Nguvava anaelezea mafanikio ya kipindi cha miaka mitano cha awamu ya tano ya Rais Dkt. John Pombe Magufuli anasema jumla ya kaya zipatozo 4,779 zimenufaika na mpango huo katika halmashauri ya wilaya ya Mbulu, baada ya kutambulika na kuqndikishwa kwenye mpango wa awamu ya tatu ya TASAF (III), na kutoka watoto 8 wa kaya masikini kujiunga na vyuo vikuu 2019-2020.

jumla ya sh. bilioni 4,073,541,260 zimetumika kuwanufaisha walengwa kwenye mpango wa huo kuanzia Julai 2015 hadi february 2019, ambapo kaya zilizopo kwenye vijiji 69 na mitaa nane za wilaya hiyo zimenufaika na mpango wa kunusuru kaya masikini kupitia mizunguko 22 ya malipo.

mnufaika wa mradi wa TASAF ambaye ni mkazi wa Dongobesh Agatha Safari (50) anasena anaishukuru serikali kwa kuwasaidia kujikwamua na maisha duni aliyopitia awali kwani alikua akiishi kwenye maisha duni kupata chakula ilikua ni mtihani kwake huku akilala kwenye nyumba ya tembe iliyowezekwa kwa majani ambapo kupitia Tasaf sasa hivi amefanikiwa kujenga nyumba ya matofari na




01

Nyumba ya mnufaika wa TASAF (III) Bi. Filimina Fransisca kabla na baada ya kunfaika

Kitengo pia kinakagua na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa taasisi na watumishi wanaojishughulisha na utoaji wa huduma kwa watoto wanaoishi mitaani na unyanyasaji kwa watoto, Vikundi hivi vinajumuisha vikundi 86 vya wanawake vyenye wanachama 430 waliokopeshwa kiasi cha Tsh 85,500,000, vijana vikundi 35 vyenye wanachama 175 kiasi cha Tsh 53,304,684.00 na vikundi 10 vya watu wenye ulemavu vyenye wanachama 50 kiasi cha Tsh 12,300,000




02

Mnufaika wa TASAF katika picha 01. Ni nyumba liyokuwa akiishi kabla ya kunufaika 02. Nyumba mpya aliyojenga na 03. Ni biashara aliyoanzisha baada ya kunufaika

# Watumishi 2893 wapandishwa cheo halmashauri ya Mbulu

HABARI KATIKA PICHA



01

Afisa utumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya mbulu Ndg. Horace Kolimba

Mkuu wa mkoa wa Manyara Mhe. Alexander Mnyeti (mwenye shati jeupe). Wakwanza kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Mbulu Mhe. Simbalimile Mofuga. Wa pili ni Mkurugenzi mtendaji Hudson Kamoga. Nyuma wa mkuu wa mkoa ni mbunge wa jimbo la Mbulu vijijini Mhe. Flatei Massay pamoja na wananchi wa Yaeda chini (Wahadzabe) katika shughuli za kiutendaji.

Serikali kupitia osifi ya Utumishi na Utawala wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu imewapandisha vyeo watumishi wapatao 2893. Afisa Utumishi na Utawala wa halmashauri ya Wilaya ya Mbulu Horace William Kolimba anasema katika kipindi hiko idara hiyo imefanikiwa mengi ikiwa ni pamoja na kuboresha kwa dawati la malalamiko, ambapo jumla ya malalamiko 5432 yamepokelewa kwa njia ya maandishi, mdomo, simu, pamoja na mtandao wa face book na kushughulikiwa, hivyo kutoa fursa ya kero za wananchi kushughulikiwa kwa wakati



02

Mkurugenzi mtendaji Hudson Kamoga (aliyevaa miwani) akikabidhi baiskeli ya magurudumu matatu (wheelchair) wa mlemavu wa miguu Marietha Qamunga ili kumsaidia katika shughuli zake. Kushoto ni motto wa mama Marietha



04

Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti amewakabidhi pikipiki watendaji sita kati ya nane wa Kata za Mjini Babati, waliokuwa wanafanya kazi zao kwa changamoto ya ukosefu wa usafiri, ili kuwafikia na kuwatumikia wananchi wengi zaidi.

"Tunasimamia stahiki mbalimbali za watumishi, likizo, matibabu, kustaafu, kuratibu shughuli mbalimbali za utawala ikiwemo sherehe, vikao vya kisheria na kupanga ratiba mbalimbali za viongozi, pia unahakikisha wananchi wanashirikishwa katika kufanya maamuzi mbalimbali kupitia vikao halali, kusomewa taarifa ya mapato na matumizi ya vijiji kila baada ya miezi mitatu na kuelezwa maagizo na mambo mbalimbali yaliyotekelezwa na serikali yao" Horace Kolimba



06

Mkurugenzi mtendaji pamoja na Mhe. Mbunge wa jimbo la Mbulu vijijini Flatei Massay wakikabidhi pikipiki kwa kwaajili ya kuwatumikia wananchi

## HABARI NA PICHA



01

Anayeongea ni makamu mwenyekiti wa halmashauri, huyu mama ni diwani wa viti maalum pamoja na watendaji wa kata na mwenyekiti wa kijiji.



02

Wajumbe wa kamati ya Bunge ya serikali za Mitaapamoja na watumishi wa halmashauri ya Wilaya ya Mbulu

"Katika kipindi cha miaka mitano jumla ya watumishi 118 wameajiriwa katika idara na vitengo mbalimbali kama vile idara ya Utumishi na Utawala, elimu ya msingi na elimu sekondari, afya na maendeleo ya Jamii" anasema Kolimba



03

Mafanikio mengine kuwa idara imefanikiwa kusimamia ujenzi wa jengo la utawala la halmashauri ambapo lililogharimu sh. bil. 4.7, litakalorahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi katika suala la usomaji wa taarifa ya mapato na matumizi kwa wananchi katika kipindi cha miaka mitano wananchi wamefanikiwa kusomewa taarifa ya mapato na matumizi kila baada ya miezi mitatu katika ngazi ya kata na vijiji, hivyo kuweka uwazi na kuongeza uwajibikaji kwa wananchi.

# Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji inavyosimamia miradi ya zaidi ya sh. Bil.6.

HABARI NA PICHA



01 Kaimu afisa mipango wa halmashauri Michael Faraay.

Kaimu Afisa mipango wa halmashauri Michael Faraay anaelezea mafanikio ya miaka mitano ya awamu ya tano Chini ya Rais Dkt. John Pombe Magufuli kuwa idara hiyo imeweza kupanga, kutekeleza na kufuatilia miradi ya maendeleo yenye thamani ya sh. bil. 6,438,612,554ikiwa ni jukumu kuu la kufanya uratibu wa miradi ya maendeleo kwa kipindi cha mwaka 2015 - june 2020.

Miradi iliyokwisha kutekelezwa na inayoendelea katika kipindi hiko cha miaka mitano kuwa ni pamoja na mradi wa ujenzi wa Kituo cha afya cha Dongobesh, ambapo serikali ilitoa jumla ya sh. mil. 400 kwa ajili ya ukarabati wa Kituo hicho ambacho tayari kimeshakamilika na kuanza kutoa huduma, ujenzi wa hospitali ya halmashauri ya Wilaya iliyogharimu sh. bil. 1.5,

ukarabati na uwekaji wa miundombinu Kituo cha afya Dongobesh, ukamilishaji wa zahanati ya Mongo wa Mono, ukarabati wa barabara ya Dongobeshb' Mnadani na Labay - Maretadu Mnadani.

Faraay anasema Miradi mingine inayoratibiwa na idara hiyo kuwa ni ukarabati wa shule ya Msingi Qaroda, ujenzi wa nyumba 31 za wakimu, ujenzi wq madarasa 29, ujenzi vyoo matundu 30, ukamilishaji wa maabara za sayansi 2, ukarabati wa soko la mazao Dongobesh, umaliziaji wa maboma ya madarasa 18 shule za sekondari, umaliziaji wabmaboma ya madarasa 8 shule za Msingi, kuchochea jitihada za wananchi katika miradi ya maendeleo kwa kutumia fedha za mfuko wa jimbo.



01 Muonekano wa ukarabati na ujenzi wa majengo katika kituo cha afya Dongobesh



03 Muonekano wa ndani wa wodi katika jingo jipya katika kituo cha afya Dongobesh

# UCHAGUZI wa serikali za mitaa 2019, CCM ilivyopasua "anga". Mbulu

HABARI NA PICHA

Afisa Kitengo cha Uchaguzi wa halmashauri ya wilaya ya Mbulu, Mkoani Manyara Michael Faraay anaelezea mafanikio ya miaka mitano ya kitengo hiko toka 2015-2020, ambapo kitengo kilifanikisha kusimamia uchaguzi mkuu 2015 wa mgombea nafasi ya Uraisi, wabunge na madiwani kuwa ulifanyika kwa amani , Uhuru na haki.

Faraay anaelezea mafanikio ya miaka mitano ya kitengo hiko toka 2015-2020, ambapo kitengo kilifanikisha kusimamia uchaguzi mkuu 2015 wa mgombea nafasi ya Uraisi, wabunge na madiwani kuwa ulifanyika kwa amani , Uhuru na haki.




02

Msimamizi mkuuu wa kitua akifuata sharia za uchaguzi kwa kubandika bango litakalotambulisha kituo cha kupigia kura



03

Mwananchi akielekezwa namna ya kuweka alama za vidole katika mashine maalum ya ukusanyaji data kwaajili ya kadi ya kupigia kura

"Matokeo ya uchaguzi wa serikali za mitaa, wagombea 1900 wa chama cha Mapinduzi (CCM) walipita bila kupingwa baada ya wagombea wa vyama vingine kujitoa katika kinyan'ganyiro cha uchaguzi kabla ya upigaji wa kura, ambapo washindi nafazi ya wenyeviti wa vijiji ni 76 (CCM), wenyeviti wa vitongoji 361 (CCM), wajumbe mchanganyiko ni 855 (CCM), na wajumbe kundi la wanawake ni 608 (CCM) " anasema Faraay

Katika zoezi la uboresha wa daftari la kudumu la wapiga kura ulifanyika juni 31, 2019 hadi agosti 6, 2019 jumla ya wapiga kura wapya 23,836 waliandikishwa, wapiga kura 8,287 waliboresha taarifa zao za wapiga kura 171 walifutwa kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo vifo, kuhama na nyinginezo, huku uandikishaji wa wapiga kura ulifanyika na kuandikisha jumla yq wapiga kura 79,662 kati yao wanawake ni 31,790 wakati wanaume ni 35,331.

Uchukuaji na urejeshaji wa fomu za wagombea uongozi Faraay anasema jumla ya wanachama 1900 wa chama cha Mapinduzi (CCM) walichukua fomu na kurejesha, vyma vingine ni CHADEMA walichukua fomu 291 na kurejesha 277, wajumbe 23 kupitia CHADEMA ndio walioteuliwa ambapo hadi kufikia Novemba 5. 2019 waiumbe 254 walienguliwa kutokana na sababu mbalimbali za uiazaii wa fomu.

# Wanaomiliki mashamba na viwanja waongezeka kutoka 186 mwaka 2015 hadi kufikia 828 mwaka 2020 Mbulu.

HABARI NA PICHA



Afisa ardhi na Maliasili Finias Kagenda

Idara ya ardhi na maliasili imefanikiwa kutoa hati miliki za mashamba na viwanja na kuongezeka kutoka hati 186 mwaka 2015 hadi kufikia 828 mwaka 2020.

Afisa ardhi na Maliasili wa wilaya ya Mbulu, Finias Kagenda anasema idara ya ardhi na maliasili ya halmashauri ya wilaya ya mbulu hadi kufikia mwezi february mwaka huu 2020 jumla ya hati miliki 828 zimetolewa kwa walengwa wa mashamba na viwanja.

Mafanikio hayo yatasaidia wananchi kuweza kufaidika na ardhi yao na hatimaye kuondoa migogoro isiyo ya lazima ya kugombania ardhi ikiwa ni sambamba na kuongeza mnyororo wa thamani wa kuendeleza ardhi husika na hatimaye kuweza kujikwamua kiuchumi kupitia Mashaka ama viwanja husika.


Mmoja wa wamiliki wa mashamba katika kata ya Yaedachini Elizabert Daniel anasema yeye amekabidhiwa hati miliki ya kumiliki shamba hivyo inamfanya awe na amani katika maisha yake kwani wapo wengine aliowasikia wakipelekana mahakamani kutokana na kudhurumiana shamaba ama viwanja, hivyo anaipongeza idara ya ardhi na maliasili kwa uwajibikaji wake wa kuwakabidhi hati miliki wananchi ama wafanyabiashara kwani hilo ni sehemu ya mafanikio makubwa sana kwani huo ndio uhalali umiliki.



01



02



Naibu waziri wa Maliasili na Utalii Mhe. Constantine Kanyasu aliyejivaa kofia nyeusi akisalimiana na wananchi wa Hydom. Mkuu wa wilaya ya mbulu Mhe. Chelestino Mofuga mwenye shati la maua. Mbunge wa jimbo la Mbulu Vijijini Mhe. Flatei Massay mwenye shuka jekundu

# Mapato ya ndani ya Halmashauri yapaa

HABARI NA PICHA

Mapato ya ndani ya halmashauri ya wilaya ya Mbulu, mkoani Manyara kupitia vyanzo vyake vya ndani yameongozeka kutoka sh. Mil.751, 985,145 mwaka 2015/2016 hadi kufikia sh. Bil. 1,289,983,759 kwa mwaka 2018/2019 ambapo ongezeko ni sawa na asilimia 72.

Mwaka hazina wa halmashauri ya wilaya ya Mbulu mkoani Manyara Respicius Kagaruki anaelezea mafanikio ya idara ya fedha na Biashara katika kipindi cha miaka mitano chini ya awamu ya tano ya Utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) Chini ya Rais Dkt. John Pombe Magufuli ikiwa hilo la uongezeko la mapato ya ndani katika halmashauri hiyo.

Kagaruki anasema wafanyabiashara katika halmashauri ya wilaya ya Mbulu nao wameongezeka kutoka 1089 mwaka 2015 hadi kufikia wafanyabishara 1481, ambapo pia halmashauri hiyo imeendelea kupata hati safi (Unqualified Opinion) toka mwaka 2015 /2016 hadi 2017/2018 ambayo hayo pia ni mafanikio makubwa kwa kushirikiana na Manejimenti na waheshimiwa madiwani, uanzishwaji wa Viwanja vidogo ambavyo pia vimesaidia kuongezeka kwa ajira mbalimbali.



01 Wafanayabiashara wakiwa katika mnada katika moja ya masoko yaliyopo Dongobesh



02 Eneo la soko katika mji wa dongobesh



03 Moja ya magari yanayotumiwa na wafanyabiashara kupita katika minada mbalimbali

"Mafanikio mengine ni kusimamia mifumo ya kihasibu ambapo kupitia Ofisi ya TAMISEMI imewezesha mifumo ya kihasibu ya malipo kufanya kazi kwa ufanisi ambayo ni mfumo wa ulipaji ngazi za chini (FFRAS ) unqotumikq katika ngazi za shule za msingi, shule za sekondari, na afya na mfumo wa Epic or unaogumika na ngazi ya halmashauri, pia mfumo wa mapato (LGCRIS) umeimarishwa kwa kiasi kikubwa sana ambao umesaidia sana kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato ya halmashauri ambapo kwa sasa vitabu vyote vimeondolewa katika matumizi ya ukusanyaji wa mapato na kusisitiza matumizi ya elektroniki katika ukusanyaji wa mapato ambao umesaidia kuongeza mapato ya halmashauri " anafafanua Kagaruki.

# UPATIKANAJI WA MAJI YA UHAKIKA HALMASHAURI YA MBULU

## HABARI NA PICHA



01



02



03



04



05

# MAFANIKIO YA IDARA YA MIFUGO NA UVUVI MBULU KIPINDI CHA JPM



Wafugaji wa halmashauri ya Wilaya ya Mbulu mkoani Manyara wanamiliki jumla ya mifugo 538,586, ambapo wameweza kuchangia kiasi cha sh. Mil. 18,734,600 kutokana na kuogesha mifugo yao katika majosho hayo ili kufanya zoezi la kogeshaji kuwa endelevu.

Afisa Mifugo na Uvuvi wa halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, Mkoani Manyara Mosses Joseph Nduligu anaelezea mafanikio yaliyopatikana kipindi cha miaka 5, 2015 - 2020 ya awamu ya tano chini ya Rais Magufuli anasema Halmashauri ya wilaya ya Mbulu imepokea dawa za ruzuku ya kuogesha mifugo kutoka serikali kuu ambapo jumla ya lita 259.5 ambazo zimegawiwa katika majosho yote 19 yanayofanya kazi, hadi mwezi February, 2020 jumla ya mifugo 538,586 iliogeshwa kati ya mifugo ipatayo 597,221 ya Halmashauri ya wilaya hiyo

Halmashauri ilitoa chanjo mbalimbali dhidi ya magonjwa mbalimbali ya mlipuko kwa mifugo ipatayo 48,039, kwa upande wa ugonjwa wa kimeta walichanjwa n'gombe 15,120, ugongwa wa kutokwa manundu /mapele kwenye ngozi (Lumpyskin) n'gombe 7,570, ugonjwa wa homa ya mapafu (CBPP ) n'gombe 23,665, ugonjwa wa miguu na midomo (FMD ) n'gombe234, ugonjwa wa Ndiganakali (ECF ) ngombe 840, na ugonjwa wa kichaa cha mbwa wamechanjwa mbwa 610.



Kwa upande wa miundombinu ya mifugo Nduligu anasema Halmashauri inayo miundombinu ya majosho ya kuogeshe mifugo 22 ya serikali huku 2 ikiwa ni ya mtu binafs ambapo mika mitano (5) iliyopita iliyokua ikifanya kazi ni mitano tu kati ya 22 ambapo kwa sasa inayofanya kazi ni majosho 19 na matatu inatakiwa kukarabatiwa na majosho mawili yataingia kwenye bajeti ya 2020/2021, malambo ya kunyweshea maji mifugo ni 15 yanayofanya kazi ni 12 na mabavu ni



Utoaji wa elimu ya ufugaji bora kwa jamii, ambapo jumla ya wafugaji wapatao 12,346 walipatiwa elimu juu ya ufugaji bora wa mifugo ikiwa ni pamoja na lishe bora kwa mifugo na kinga dhidi magonjwa ya mifugo.

Hata hivyo kwa upande wake mfugaji maarufu katika bonde la Yaeda chini Yonas Assecheck anaipongeza serikali ya awamu ya tano inayoongozwa na Rais Magufuli kwa kuijali mifugo, kwani nao wamepata nguvu katika kuendeleza ufugaji wenye tija utakaowaletea maendeleo ya kujikwamua